Fedha au mahari?

Hadithi kutoka Kenya,

Mfalme mmoja tajiri alikuwa na binti mmoja tu. Watu wengi wenye majumba, ardhi na mifugo wengi waliomba wamwoe. Lakini pia kulikuwa na maskini mmoja ambaye naye alitaka kumwoa. Mfalme huyo alikuwa na hekima. Akaamua kuwapa mtihani ili apate mtu ambaye angemfaa bintiye.

Credit: Intermediate Technology Publications

Siku moja maalum, alimvika bintiye nguo zenye mifuko mingi na alijaza fedha katika mifuko hiyo. Wale watu waliotaka kumwoa walijipanga mstari na mfalme akamwambia binti yake akimbie na watu wale wakaanza kumfukuzia. Walipomkaribia alichomoa furushi la fedha toka mfukoni mwake na kuwatupia. Kwa hiyo matajiri walipomkaribia walisimama ili waokote fedha, na yule binti akiendelea kukimbia mbali. Lakini yule maskini hakujali zile fedha bali alimfuata yule binti hadi akamkamata. Mtihani ulipokwisha, yule maskini alipewa fedha nyingi na ardhi toka kwa mfalme na pia alipewa yule binti awe mke wake na wote walikuwa na furaha.

Sasa fikiri:

- Je, maisha yetu ni sawa na shindano la mbio? Ni kwa nini?
- Je, ni vema kukimbiza nini katika maisha yetu?
- Je, katika maisha yako ni kitu gani muhimu sana? Kinakupa furaha?
- Ni watu gani katika hadithi hii ambao ni huru?
- Je, uhuru wa kweli ni nini?
- Je, ni nini tulicho nacho maishani kinachotuzuia kupata kitu chema?
- Je, kuna hatari yoyote katika fedha?
- Yule maskini alipokea kila kitu bure. Hakulipa mahari yoyote. Je, Mungu anapenda kututendea hayo hayo?

Katika 1 Yohana 2:15, 17 tunasoma, **"Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele."**

(Kwa hisani ya Good News Publication International, Africa)

YESU alisema: Naja—

upesi

Ufunuo 22:12

Nimepewa huru

na *Kevin Mills, Uingereza

Nilikuwa ni mmoja wa kundi la majambazi na pia nilizoea sana kutumia madawa ya kulevya, kwa hiyo fedha nilizoiba nilizitumia kununulia hayo madawa. Nimepoteza ncha ya kidole gumba cha mkono wangu wa kushoto kwa kujigonga kwa nyundo nilipokuwa nikifungua sanduku la chuma la kuwekea fedha. Nikiwa na umri wa miaka kumi na tano tu.

Siku moja nilipigana na watu wabaya na polisi wakaja na kunikuta nimelala barabarani. Walijua kuwa nilikuwa nimefanya maovu mengi. Kwa hiyo walinipeleka Dartmoor ambako ni gereza linalofahamika sana nchini Uingereza. Huko nilifungwa kwa saa 23 kila siku katika chumba kidogo cha hiyo gereza.

Miaka sita baadaye nilitoka gerezani huru lakini sikuwa huru na madawa ya kulevya pamoja na hamu ya kuumiza watu. Jambo la kwanza nililofanya ni kupata bunduki kwani nilitaka kuwaua wale watu niliopigana nao. Niliwaagiza rafiki zangu tukutane katika kituo cha treni wakiwa na hiyo bunduki. Badala ya kuleta bunduki, walininiletea mama yangu. Mama alisema jambo moja tu, *"Kevin, unahitaji kubadilika."* Jambo hili lilinifikirisha sana.

"SIWEZI KUYATUMIA TENA"

Siku moja nilipokuwa nikijidunga sindano na madawa kwenye mkono wangu nikawa ninasema, *"Siwezi kuyatumia tena."* Rafiki zangu waliangalia ng'ambo ya barabara, wakanishauri tuingie katika nyumba ambayo ilikuwa karibu. Hapo kulikuwa kanisa ambako watu hukutana ili waabudu Mungu. Kikundi hicho kiliitwa Betel. Watu hawa walifanya kazi ya kurekebisha maisha ya watu hasa wale walioathirika na madawa ya kulevya.

Mnamo Septemba 1998 nilienda kukaa katika nyumba ambayo ni kituo cha Betel. Rafiki zangu waliniambia kuwa nisingekaa hata wiki mbili lakini nilipenda kufanya kile mama alichonishauri. Nakumbuka nilipokuwa nikiingia mlangoni nilitambua kuwa kila mtu alikuwa na furaha, nami niliweza kuusikia upendo wa Mungu. Niligundua kuwa watu hawa walikuwa hapo mwanzoni kama mimi, yaani maisha yao yalikuwa mabaya bali wamebadilika.

Wakati huu sikupenda kuwa Kevin yule ambaye amekuwa hivyo kwa miaka mingi, kwani nilitamani nisikie furaha ndani yangu. Saa tisa kamili za usiku sikuweza kulala. Asubuhi yake nikayatoa maisha yangu kwa Yesu.

NILIANZA KUJIFUNZA

Wakati huu ndipo nilipoanza kujifunza kuwa naweza kumwomba Yesu anisaidie katika matatizo yangu. Kumjua Mungu na kumwamini kulinipa amani. Je, ningeweza kupata wapi tena uhuru huu katika maisha? Ni kwa Yesu tu. Kwa kweli ni maajabu Mungu aliyoyafanya katika maisha yangu. Ninamshukuru na ninampenda. Nimekuwa nikifanya kazi India kuwasaidia watu watumiao madawa ya kulveya ili waweze kuujua uhuru nilioupata.

**Ingawa siyo jina lake halisi*

Ushuhuda wangu

Boniface Mlondera, Tanzania

Mimi ni kijana mdogo niliyebatizwa mwaka wa 1986. Baada ya kubatizwa nilianza kupatwa na shida nyingi na vishawishi. Mwaka 1987 shetani alijaribu mara nyingi kuniangusha kwa ugonjwa. Niliendelea kuwa na shida za kila aina kwa sababu nilikuwa mchanga kiimani na kwa hiyo niliamua kwenda kumwona mganga wa kienyeji.

Baada ya hapo nilianza kazi ya uvuvi. Nikazidi kusongwa na shida nyingi kazini. Nikaamua kwenda tena kwa mganga wa kienyeji, naye aliniambia nizike fedha kadhaa aridhini ili niweze kufanikiwa. Roho yangu ilidhoofika sana lakini Yesu alinihurumia naye akaniosha na kunitoa balaa zote. Namshukuru Mungu kwa sababu ameniita na kunipa nguvu ya kuishi karibu naye.

"Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa. Kwa maana, ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara, na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki, sisi je! Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia;" (Waebrania 2:1-3.)

Kata hapa

Jina .....No 87/.....

Anwani.....

.....

Nchi .....

KUPOKEA NAKALA YA UPESI BILA MALIPO, andika jina na anwani yako hapa kwa HERUFI KUBWA. Tuma kwa:

UPESI, Box U,
44 Twyford Road
Willington, Derby
England, DE65 6BN

(Ukituma barua bila stampu, au ukitia stampu zisizo mpya, barua haitatumwa.)

Ukitaka kusoma UPESI kwa INTERNET, tumia: http://soon.org.uk/swahili/swahili.htm

ISSN 1472-7285

Kwa Mhariri wa UPESI,

Sijui hata jinsi ya kuelezea shukrani zangu kwenu. Sikuamini kama gazeti hili lingenipa tumaini.

Tarehe 23 Julai 2000 nilitaka kufa, mzigo wangu uliniwia mzito mno hata kupoteza tumaini. Sikufahamu nifanye nini, sikuweza kula au kufanya kitu chochote kwa sababu moyo wangu ulikuwa na uchungu. Niliamua kwenda kwa rafiki yangu ili anisaidie kutatua matatizo yangu. Nikiwa njiani kuelekea kwake, nilisimama kwenye afisi ya posta kuangalia kama nilikuwa na barua toka kwa kaka yangu. Kitu nilichokuta kwenye sanduku la posta kilikuwa kikaratasi tu kiitwacho UPESI. Nilililfungua gazeti hilo na kulisoma, nami sikufahamu ni wakati gani machozi yalipoanza kutiririka usoni. Nilijiona kama mwenye dhambi na nikamwomba Mungu pale pale kwenye afisi ya posta.

Tangu siku ile mambo ambayo sikuyategemea yalianza kujitokeza kwangu, kwa mfano, hali yangu kimasomo iliboreka. Naamini Mungu wetu yu hai na ana mpango kwa ajili ya kila mmoja wetu.

Wako mwaminifu,
Solomon O. Enyosiobi,
Nigeria.

Barua kutoka Kwa wasomaji

Kwa Mhariri wa UPESI,

Nilikuwa mwenye dhambi mkubwa, kwani nililala na wasichana na matokeo yake nilimpa msichana mimba. Baba yangu ambaye ni mchungaji, amepoteza mbuzi na fedha nyingi kwa sababu yangu. Niliposoma karatasi ya UPESI nilifahamu waziwazi jinsi nilivyofanya vibaya.

Katika karatasi ile nilikuta sala hii, *"Bwana Yesu, nimeishi jinsi nilivyotaka na kukukosea wewe. Naomba unisamehe, nakufungulia mlango wa maisha yangu; nakupokea uwe Bwana na Mwokozi wangu. Yesu Kristo, nakushukuru kwa kuwa umenisamehe dhambi zangu. Naomba unipe uelekeo wa maisha yangu; naomba unisaidie kulifahamu pendo lako."*

Nilimtenda Mungu dhambi sana lakini sala hii imenisaidia sana.

Nakusalimia katika Kristo,
Acruma Tarabe,
Dem. Rep. of Congo

Kwa Mhariri wa UPESI,

Mimi ni kijana wa umri wa miaka 18 na kwa muda mrefu sasa nimesoma gazeti lenu. Walakini niliamua kumwamini Yesu mwaka jana tu. Kabla sijampokea Yesu nilikuwa kiongozi wa chama chetu cha vijana cha dini. Sikuwa tu msomaji wa mambo ya dini, bali pia nilikuwa mjukuu wa kiongozi mkuu wa dini katika jamii yetu. Nilipokuwa mwanafunzi wa sekondari, nilianza kufahamu habari za Yesu. Kwa sababu nilikuwa kati ya wapinzani wakuu waliokuwa wanahubiri kinyume cha Ukristo, sikuweza kudhihirisha upendo wangu kwa Yesu mpaka hivi karibuni.

Nilipoanza kutafsiri maandiko ya kikristo toka kiingereza kwenda kwenye lugha yetu, habari zilifikia familia yetu. Kwa sababu hiyo nilifukuzwa nyumbani na baba yangu akakataa kulipia masomo yangu ya chuo kikuu. Namwomba Mungu kuwa nitapata msaada na kuendelea na masomo yangu.

Wako katika Kristo,
Adam,
Ghana

Kufuma vitu vya thamani

Mhariri wa UPESI

Mifuko ya plastiki imetapakaa kila mahali nchini mwetu. Hii mifuko hutokana na ununuzi wa vitu kutoka madukani. Mara baada ya kuondoa vitu hivyo, mifuko hiyo hutupwa ovyo barabarani au katika malundo kwa maelfu. Kutoka hapo huchukuliwa na upepo na kutapakaa njiani na katika mashamba na malisho. Hali hii huharibu sana mazingira kwa vile mifuko hii haiozi, kwa hiyo ng'ombe, mbuzi au wanyama wa porini wanapoila haiyeyuki tumboni kwa hiyo wanyama hufa taratibu na kwa maumivu makali.

Katika nchi ya Niger watu wamejaribu kufuma kamba kutokana na mifuko hiyo ili wafunge wanyama wao. Hao waligundua kuwa wangeweza kutengenza kamba imara sana hata zingewaumiza wanyama. Hatimaye wakajifunza kufanya kamba ambazo zitumiwa kufuma magunia au hata viti vya kukalia.

MAMA ANAFUMA KOFIA

Huko Afrika Kusini, mama mmoja akaaye katika kambi fulani hufuma kofia, magunia na mikeka kutokana na mifuko ya plasitiki. Huikata mifuko hii katika kamba nyembamba ambazo husukwa vizuri. Watu wengi wavaao kofia zake wanashangaa kuwa siyo za joto hata kama jua ni kali sana. Kofia hizo ni rahisi kuosha tu kwa sabuni na kitambaa, kisha kusuuzwa na hatimaye kuanikwa juani zikauke. Magunia na

mikeka pia yadumu kwa muda mrefu. Huuzwa kwa bei rahisi na pia ni rahisi kufuma.

Fedha kidogo tu itahitajika kuanza kazi kubwa. Watoto wa mitaani huweza kuajiriwa kukusanya mifuko hiyo ya plasitiki njiani. Watoto hao wanaweza kutumiwa kuuza kofia, mikeka, magunia au viti (au chochote unachokifuma kutoka kwa mifuko hiyo) katika mitaa au sokoni au hata katika maduka.

Mifuko hiyo ya plastiki isiyokuwa na thamani, huweza kutengenezwa kuwa kitu cha faida kinachodumu na kutumiwa sana. Yesu humpokea mtu ye yote kumbadilisha awe mwenye thamani kwa kufaa kutumiwa na Mungu, na pia Yesu humpa uzima wa milele. Ila yatubidi tumwombe tu. **"(Mungu) humwinua mnyonge kutoka mavumbini, na kumpandisha maskini kutoka jaani. Amketishe pamoja na wakuu, pamoja na wakuu wa watu wake".** (Zaburi 113:7,8.)

"Ramon Amebadilika"

na Ramon, Argentina

Watu walisema, *"Tunamwogopa sana, kwa sababu anakunywa sana pombe na kutumia madawa ya kulevya. Huyo anaweza kukushambulia kama ukikutana naye njiani."* Ndivyo walivyosema juu yangu. Siku moja polisi walinikamata, na nilipofikishwa mahakamani, hakimu alisema, *"Unahukumiwa kwa makosa 28, nawe utaenda gerezani kwa muda mrefu."*

Siku moja nilijaribu kuteketeza gereza kwa moto. Nikasumbua sana kule gerezani na watu wakashindwa kulala; wakisema, *"Huyo ni kichaa."* Siku moja watu watatu waliwekwa katika chumba nilichokuwamo. Watu hao walikuwa na tofauti kabisa kwa sababu hawakutumia pombe, madawa ya kulevya wala hawakusema maneno mabaya.

NILISAIDIA WATU GEREZANI

Waliniambia, *"Twende kwenye mkutano katika gereza hilo."* Katika mkutano ule, mtu mmoja aliomba akisema, *"Ee, Mungu badilisha maisha ya Ramon."* Alipoomba hivyo, pepo wachafu walipiga kelele huku wakikataa kuniacha. Walakini Roho ya Mungu aliwatoa ndani yangu. Baada ya hayo kila mtu aliyeniona alikiri, *"Ramon amebadilika."*

Kisha Mungu alinitumia kuwasaidia watu walioko gerezani kupokea kipawa cha Roho ya Mungu. Mungu alitenda kazi hadi watu 1400 walikuwa wakija katika mikutano yetu kule gerezani. Tangu nilipotoka gerezani Mungu amekuwa akinitumia kusaidia watoto wengi wa mitaani katika mitaa ya La Plata.

Sikiliza Redio!

Kupokea Habari Njema katika lugha ya Kiswahili kwenye **Redio FEBA** kwa **Redio Habari Maalum** sikiliza 11885 kHz, Mitabendi 25 kila siku:
Asubuhi: Saa 12 na robo;
Usiku: Saa 1 na robo.
TWR: 5970 kHz, MB 49: Saa 12 kila asubuhi; 9440kHz, MB 31: Saa 2 kila usiku.
Mombasa-**Baraka FM** - Kwenye 95.5FM katika Kiswahili kwa Kiingereza.

Jifunza kitabu cha Mungu

Ukitaka kupata Masomo ya Biblia katika lugha ya Kiswahili kwa posta, tuma jina lako na anwani yako kwa:

Katika KENYA: Emmaus Shule ya Biblia, SLP 72725, Nairobi, Kenya.

Katika CONGO: Cours Biblique Emmaus, BP 350 Bunia, Rég. du Haut-Congo, Rép. Dem. du Congo.

Katika TANZANIA: Emmaus Shule ya Biblia, SLP 1424, Dodoma, Tanzania inasubiri barua yako ili uweze kutumiwa somo la kwanza bila malipo.